# STD 5 END TERM 2 EXAM 2019

## KISWAHILI

*Soma vifungu vifuatavyo. vina nafasi* **1 - 15.** *Katika kila nafasi, umepewa majibu manne. Chagua jibu lililo sahihi kati ya yale umepewa.*

Watu wengi hawapendi __1__ kazi __2__ wanaogopa kuchoka. Wanapenda __3__ vitu vya bure __4__ hawakuvichokea. Lakini __5__ ni kitu muhimu kutokana __6__ tunapata __7__. Nchi __8__ na maendeleo, __9__ hupata maendeleo __10__.

Mchwa wanaweza __11__ kama mfano. Wadudu __12__ hufanya kazi __13__ bidii bila uvivu kila __14__ huwa na kazi __15__ ya kufanya.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. kufanya | B. wanafanya | C. hufanya | D. walifanya |
| **2.** | A. halafu | B. ili | C. kwani | D. au |
| **3.** | A. kupatilia | B. kupata | C. kupate | D. kumpata |
| **4.** | A. ambayo | B. ambao | C. ambalo | D. ambavyo |
| **5.** | A. kazi | B. makazi | C. mkaazi | D. kasi |
| **6.** | A. nawo | B. nayo | C. nao | D. naye |
| **7.** | A. faida | B. fuadi | C. fida | D. fani |
| **8.** | A. hui | B. huwa | C. huwi | D. haliwi |
| **9.** | A. wananchi | B. wanainchi | C. wanachi | D. wananji |
| **10.** | A. wengi | B. nyingi | C. mengi | D. tumiwa |
| **11.** | A. kutajiliwa | B. kutumiwe | C. kutumiwa | D. tumiwa |
| **12.** | A. hawa | B. hii | C. huyu | D. huu |
| **13.** | A. kama | B. na | C. kwa | D. wa |
| **14.** | A. mumoja | B. mmoja | C. moja | D. kimoja |
| **15.** | A. yake | B. wake | C. lake | D. chake |

*Chagua jibu sahihi kujibu maswali* **16 -30.**

**16.** Fundi wa mbao huitwa
A. fundi
B. mhunzi
C. mwashi
D. seremala

**17.** Istiara ifuatayo ina maana gani; Kanati ni chiriku.
A. Anaimba
B. Anaiga
C. Anasema sema
D. Anapenda

**18.** Kamilisha methali hii: Mgema akisifiwa tembo hutia
A. maji
B. maziwa
C. uji
D. mchanga

**19.** Kipeto ni cha barua nayo thureya ni kwa
A. mwezi
B. nyota
C. moto
D. pamba

**20.** Kitendawili: Tega: Popoo mbili zavuka mto
A. Samaki
B. Macho
C. Ndovu
D. ndege

**21.** Dereva wa gari moshi huitwa?
A. Kandawala
B. Kapteni
C. Dereva
D. Nahodha

**22.** Kamilisha kwa wingi: Minofu ile ______ itakayoliwa.
A. ndizo
B. ndilo
C. ndiyo
D. ndio

**23.** Mlinzi wa langoni huitwa:
A. kufuli
B. bawaba
C. baba
D. bawabu

**24.** Nywele nyeupe ziotazo kichwani huitwa
A. pamba
B. mvi
C. mpingo
D. jivu

**25.** Chakula cha mchana ni
A. kishuka
B. kisebeho
C. kerbu
D. chotara

**26.** Wingi wa saa ni
A. visaa
B. lisaa
C. masaa
D. saa

**27.** Kikembe cha nyuki huitwa?
A. Kinda
B. Jana
C. Kelbu
D. Chotara

**28.** Kanusha: Amenuna
A. Amecheka
B. Hacheki
C. Hajanuna
D. Ametabasamu

**29.** Paka ni kwa manyumba ilhali kasa ni kwa
A. wayo
B. gubeti
C. matendegu
D. kucha

**30.** Ni nomino gani si kati ya A-WA?
A. Kinyonga
B. Nyigu
C. Mbuni
D. Makochi

***Soma kifungu kisha ujibu swali la 31 – 40***

Mama Kazungu hakuwa kipofu alipozaliwa. Alikuwa mtu wa kawaida mwenye macho mawili. Kwa kweli alikuwa akiona mbali sana. Baada ya siku kadhaa, miezi na miaka kuisha, mama Kazungu akawa **kipofu** huku akiwa na macho yake.

Baada ya dhiki faraja kama ilivyosemwa na wazee wa zamani, mama Kazungu hakufaidika. Aliishi katika dunia ya dhiki au taabu. Alizaliwa katika hali ya umaskini na baadaye akaolewa na mume fukara au maskini hohehahe. Aliishi na mume wake kwa miaka saba. Bwana fukara yaani mumewe mama Kazungu aliaga dunia akiwa na mtoto wa miaka sita. Mtoto huyu aliitwa Taabu.

Taabu hakuweza kuendelea na masomo yake kwa sababu hakuwa na karo. Alipofika darasani, aliwakuta wenzake wakiwa na kalamu za wino, kalamu za risasi, madaftari, rula, vifutio na hata vichongeo. Yeye hakuwa na vitu hivyo vyote. Wanafunzi wengine walimwonea huruma. Walimu pia walimwonea huruma lakini kwa shida nyingi, huyo mtoto aliacha shule akiwa katika darasa la tatu muhula wa pili mwaka wa elfu mbili na tisa.

**31.** Mtu asiyekuwa na uwezo wa kuona huitwaje
A. kiziwi
B. kibofu
C. maskini
D. kipofu

**32.** Ni nini baadhi ya vitu hivi havijatajwa kwenye taarifa?
A. rula
B. gari
C. penseli
D. kalamu

**33.** Wanafunzi na walimu walimwonea Taabu nini?
A. wivu B. kijicho
C. huruma D. woga

**34.** Mtoto wa mama Kazungu alihitaji kulipa nini ili asome?
A. karo
B. nauli
C. mshahara
D. kiingilio

**35.** Mumewe mama Kazungu alikuwa akiitwa
A. Bi. Fukara
B. Bw. Fukara
C. Taabu
D. Kazungu

**36.** Mtoto wa mama Kazungu aliacha shule akiwa darasa gani? La
A. pili
B. tatu
C. nne
D. kwanza

**37.** Mama Kazungu alizaliwa katika hali ya
A. bure B. ujuzi
C. umaskini D. utajiri

**38.** Taabu aliacha shule katika mwaka wa elfu
A. mbili na tisa
B. mbili na sita
C. moja na tisa
D. mbili na tisa sita

**39.** Nomino **kipofu** limepigiwa mstari. Wingi wake ni
A. pofu
B. viipofu
C. vipofu
D. vipovu

**40.** Ni kiumbe gani hakijatajwa katika habari hii?
A. Mama
B. Wanyama
C. Mzee
D. Wanafunzi

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali* 41 – 50**

Kusali kabla ya chakula chochote ni kwema. Ilikuwa Jumamosi jioni tulipoandaliwa chakula mezani. Siku hii ilikuwa zamu yangu kumwomba Jalali. Haifai kula chakula kabla ya kuomba.

Kwanza tulinawa mikono ili kutoa uchafu. Chakula kilipowekwa kwenye meza, nilimsihi kila mmoja ainamishe kichwa na afumbe macho. Hapo ndipo nilianza kuomba, "shukrani mbele ya chakula. Bwana juu na chini, tubariki mezani , pamoja na cha mwili, utupe na cha roho pia. Amina!"

Kwa wakati huu, hakuna nzi au paka aliyekaribia chakula kwa kawaida, baba huanza kupakua chakula akiwa wa kwanza. Kisha kitinda mimba wetu jokoyo hufuata halafu mimi, kisha mama yangu huwa wa mwisho.

Tulipoanza kula, tulikumbushwa kuwa si tabia njema kula haraka na kwa pupa kama nguruwe. Huo ni ulafi na ulafi ni wa fisi. Pia si vyema kah[illegible] kujaza mafunda au matonge makubwa makubwa kinywani na kuanza kuongea huku watu wakik[illegible] a chakula mdomoni. Kwa kweli haifai katu!

Tabia njema ni kutia chakula kiasi mdom[illegible] kukitafu[illegible] isha kukimeza bila kusakamwa au kukabwa koo.

Mwisho mama alisema, "tukiwa mezani tu[illegible] ibu kusema chakula ni kibaya, kwani ni kumtukana mpishi."

**41.** Ni sehemu gani ya mwili mtu huinawa na si kuoga?
A. Kiwiliwili cha mwili.
B. Uso na mkono.
C. Kichwa
D. Kifua

**42.** Kula haraka haraka tunasema ni
A. kutumia muda ifaavyo.
B. kushiba.
C. tabia njema.
D. kula kwa pupa.

**43.** Ni neno gani halikaribii maana ya neno kusali?
A. kuazima
B. kumshukuru
C. kuabudu
D. kuomba

**44.** Ugali kipande kikubwa huitwaje?
A. funda la ugali
B. kipande cha ugali
C. tonde la ugali
D. kigaro cha ugali

**45.** Kuweka chakula mezani ili kiliwe ni
A. kudanganya
B. kuweka chini
C. kutandika mkeka mezani
D. kuandaa meza

**46.** Ni nani aliyesema ombi kulingana na taarifa hii?
A. Mjomba
B. Mzazi baba
C. Mwandishi
D. Mzazi mama

**47.** Ni wakati upi tunastahili kula chakula
A. baada ya kukiombea
B. kabla ya kukiombea
C. wakati wa kukila
D. kabla na baada ya kukiombea

**48.** Tunasema mnono kama nguruwe ilhali mlafi, kama
A. mbwa
B. fisi
C. nguruwe
D. mwenye pupa

**49.** Hali ya kukitoa chakula kwenye sufuria au chano na kukitia kwenye sahani tayari kukila ni
A. kuinjika
B. kupatiana
C. kula
D. kupakua

**50.** Ni orodha gani sahihi ya waliopakua chakula kuanzia wa kwanza hadi wa mwisho?
A. Mama, jokoyo, baba, mimi.
B. Baba , mimi, jokoyo, mama.
C. Mama, kitinda mimba, mimi, baba.
D. Baba, kitinda mimba, mimi, mama.

JESMA DECEMBER HOLIDAY HOMEWORK BOOKLETS FROM ECD TO CLASS 8 WILL BE